Jiwe la kiroho la kujengea No.109.

# Udhihirisho wa mawazo ya Mungu

Mt.Yohana1:1-3``*Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye neno Alikuwako kwa Mungu,naye Neno alikuwa Mungu.``*

*Naye neno alikuwa ndani ya Mungu;alikuwa Mungu,ilikuwa ni mawazo yake aliyokuwa nayo siku zote.mawazo ya Mungu ni ya milele kama Mungu alivyo.Amina!*

Hapa linakuja! Mawazo ya Mungu yalikuwa Neno lake.``Hapo mwanzo---``(Hayo yalikuwa Milele sasa,hapo mwanzo ulipoanza,muda)---``Hapo mwanzo kulikuwako neno…``(mawazo ya Mungu)…``unaona?mawazo yake ndicho alicho kuwa.ndivyo na wewe pia vile mawazo yako yalivyo ndivyo ulivyo.

Haijalishi unajaribu kuishi kwa kitu Fulani kingine,mawazo yako ndicho ulicho. Unaweza ukaigiza kutenda kama mtu mzuri,lakini moyoni mwako ni mzinzi,na chochote kiwacho,ndivyo ulivyo…mawazo yako na mawazo ya Mungu yalikuwa Neno lake,lililokuwanaye na ndani yake,na ilikuwa ni Mungu.

Na kila mwaminio anayekuja kwa Yesu lazima aje msalabani palepale pa kujikana-mwenyewe,na afe pale na mwanakondoo,na kondoo wake.afe kwa mawazo yake mwenyewe;afe kabisa kwa mawazo yake ya kiakili achukue kile tu Roho mtakatifu anachosema moyoni mwako,halafu kuishi kwa kristo.

Na sasa,``Neno`` ni wazo lililo dhihirishwa``kwanza,inabidi iwe ni mawazo,na halafu inakuwa Neno;kwa sababu huzungumzi maneno yako bila mawazo.

Tunaponena kwa lugha,hatuna mawazo(1kor.14:13-14); ni Mungu akichukua mawazo;ni mawazo ya Mungu alitumia midomo yetu;hatufikirii au hatujui kile tunachosema,tukinena kwa lugha, au kile kunena kwa kuvuviwa.unapotafsiri hujui kile unacho sema;unasema tu;hivyo tu;hivyo tuu unaona.huyo ni Mungu. Na kutoa unabii,hutumii mawazo yako mwenyewe,ni Mungu(1kor.14:1-3),kwa sababu unasema mambo ambayo kwa kawaida usinge fikiria kusema hayo.

Kwa hiyo,Hapo mwanzo kulikuwako neno''hapo ndio umbali tuwezao kwenda nyuma ,kwa hii, theologia.lakini kabla ya neno



kuwako,ilikuwa ni wazo, na wazo lilidhihirishwa.unaona ninacho maanisha?sasa,hivyo dhivyo alivyosema mwanzo,alifikiria,na akanena neno ,na Neno lika dhihirishwa.oh vile Mungu asivyoweza kukosea angalia,kila wazo pale linaponenwa.

Na kila neno katika Biblia ni wazo la Mungu likiwa katika hali ya mbegu,kwamba kama litapokelewandani ya mtu, na likanenwa kwa wazo lilelile lililo fanya Biblia iandikwe, itafanya jambo lilelile litendeke, unaona kile ninacho maanisha?vile kanisa liwezavyo kuwa na nguvu nyingi?Biblia ilisema,``iweni na nia ileile ndani yenu nia iliyo kuwa ndani ya Kristo(Wafilipi2:5)vile mtu awazavyomoyoni mwake,ndivyo alivyo(mithali23:7)```sasa mawazo yako kama yatadhihirishwa---

Kama Mungu alivyosema,``naiwepo dunia``(Mwanzo1:3-26)kabla ya kuwa Neno,ilibidi iwe ni wazo.kwa hiyo Mungu katika uumbaji,aliumba ulimwengu kwa mawazo yake kwanza,halafu akanena hilo na lile wazo,lilipo dhihirishwalikawa kitu halisi,unaona ninachomaanisha?

Sasa, kama roho yuleyule aliyesema,``iwe nuru`` na ikawepo nuru''iwepo miti'' na ikawepo miti;na kama nia ileile iliyokuwa ndani ya Kristo iko ndani yako,itasema kwa kiasi gani, ''kusiwepo(kensa)saratani tena''na itakuwa imeondoka;''macho yaliyopofuka yaone,'' na itakuwa hivyo.unaona? ni mawazo yako.Yesu alisema,''Amina…''

Unasema,''huyo alikuwa Yesu'' lakini subiri kidogo.Alisema ''mwaminini Mungu.Amini,amini nawaambia yeyote atakaye wambia mlima huu,ng'oka ukatupwe baharini asione shaka moyoni mwake,ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia,yatakuwa yake,''hiyo ni sawa?yatakuwa yako''ni nguvu ya jinsi gani iliyopewa kanisa….(Mark11:22-23)

Sasa,unaweza kulielezea kwa mawazo ya kiakili,lakini kama itakuwa ufunuo halisi wa Mungu,kwamba unaliona hilo kabla halijatokea,na kulieleza kwa namna ya Neno,na hilo neno likashikilia na kuwa udihirisho wa kitu;wazo lilidhihirishwa.oh jamani,jinsi Mungu awezavyo-----unaona?kama moyo wako na nia yakoviko hivyo,na kujanzwa na roho wa Mungu,mpaka mawazo yako yakawa ni mawazo yake---Amen.unaona hilo.wakati nia yako,uongozi

wako,nakiongozi wako,wikawa ni mahali pa wazi,au mahali pa uvuvio wa dhahiri wa Roho Mtakatifu ambaye anauendesha utu wako unaokufa…oh jamani.

Tutakuwa watu wa namna gani?kama Roho mtakatifu mwenyewe ameungana nawe au kututia nguvu,kwamba hutumii mawazo yako mwenyewe,hutumii akili(nia)yako mwenyewe, hutumii mashauri yako mwenyewe;lakini Roho mtakatifu amekujenga wewe,mpaka mawazo yako utu wako ni Roho wa Munguakijidhihirisha/kujieleleza mwenyewe kupitia wewe,tutakuwa kanisa la namna gani?

Tungekuwa watu wa aina gani,asubuhi hii ya leo,kama maskani haya ya Branham,asubuhi hii,yangekuwa yamejazwa na uwepo wa mungu,kwa nini?ulikuwa hukutumia akili zako mwenyewe,hukuwa nakitu badala cha kwako mwenyewe,lakini huongozwa tu na Roho…?

‘’na walewalio wana wa Mungu wanaongozwa na roho wa Mungu’’(Rumi8:14). Sasa ile haliya kibinadamu iliondoka,na Roho wa Mungu anajaza hilo pengo/au hiyo nafasi,mahali ambapo unajimwaga mwenyewe(Amen),hiyo italifanya kanisa liwe katika nguvu zake za kufufuka kwake Bwana Yesu,litatembea katika hatua zake,katika mawazo yake,katika utu wake,katika utendaji wake…unaona kile ninacho maanisha?hapo sasa mawazo yako yatakuwa Neno,na Neno litakuwa kitu kinachoonekana.hapo ndipo kanisa litakuwa katika nguvu zake

naamini liko njiani linakuja,hapo sasa kanisa litakuwa limefungwa ndani ya Kristo,Roho mtakatifu, mwanadamu anakuwa nje na ya kwake mwenyewe kiasi kwamba hajioni mwenyewe,hawana mawazo ila kumtumikia Mungu.na mawazo yao yanaendelea,wanakataa mambo/vitu vya dunia.wanaenenda kwa Roho,wanaishi kwa Roho,wanatenda kwa Roho,wanatembea kwa Roho,kuitimiza sheria ya Kristo.sasa upendo wa Mungu katika moyo wa mwanadamu(warumi5:5), wakitenda katika Roho mtakatifu, lile kanisa kuu la ajabu litaenda hivyo katika nguvu za uungu;kwa sababu uungu utakuwa unafunuliwa ndani ya mwanadamu kwa Roho mtakatifu na kuyafanya kutimia mawazo ya nia zao.

Mawazo yetu yanakuwa tofauti;mara nyingi tunatembea na kusema,``uhali gani,ndugu?``na humaanishi hilo ndani ya moyo wako.mara nyingi tunasema``niko hivi na vile.nitafanya hivi.``humaanishi hivyo ndani ya moyo wako.unaona?simaanishi hilo moyoni mwangu.



Lakini unapokuwa umekufa katika mambo ya dunia,kwamba Kristo ana nafasi ya kwanza,Kristo ni yote hapo sasa utu wako wote umeumbika kwa Roho wa Bwana Yesu kristo,yeye anakuongoza kikamilifu.hapo ndipo mawazo yako yatakuwa safi.mawazo yako yatakuwa yasiyo changanywa

Watu wengi wanasema,``vema,dini inatoka moyoni mwako``hakuna mawazo ya kiakili katika kile kitu kidogo kiitwacho``moyo``huwezi ukafikiri kwa moyo wako.Biblia ilisema,``kama vile mtu awazovyo ndani ya moyo wake,ndivyo alivyo``huwezi ukafikiri kwa moyo wako.huwezi kwasababu hakuna kitu cha kiakili pale cha kufikiri nacho.Yesu hakuwa anazungumzia utu wa kuonekana;alikuwa anazungunzia utu wa kiroho.``kama mtu afikirivyo…..``lazima iwe ni wazo kwanza kabla ya kuwa neno.na neno lililodhihirishwa,linakuwa kitu kinachoonekana.ninaamini moyoni mwangu kwamba mimi ni mkristo,kwasababu nimempokea Bwana Yesu Kristo;kama sikulia,kama sikusogea kama sifanyi lolote,moyoni mwangu kwanza,ninaamini kuwa kristo alikufa na kuchukuwa mahali pangu. Amina.ninalikubali hilo kama mkristo;ninaliamini hilo kama mkristo,na halafu kiko moyoni mwangu.halafu ninalieleleza kwa neno,``kuwa mimi ni mkristo,``halleluya.halafu ninaanza kutembea kama mkristo.ninazungumza kama mkristo,ninaishi kama mkristo ninakuwa kama mkristo –na kwa matunda yangu,nitatambuliwa na dunia kama mkristo,haleluya.

Tu wakristo kwa imani kwa neema ya Mungu tuwakristo(waefeso2:8-9). Unaona?Mungu katika wingi wa huruma zake,alituita tupatanishwe nayekupitia mwana wake KristoYesu.linamaliza hilo.siyo tulicho fanya,ni alichofanya;amebadilisha nafasi yangu kutoka mambo ya dunia kuja kwenye mambo ya Mungu,kutoka kwenye mashindano ya farasi,na kamari na uzinzi,uongo na wizi,amebadilisha nafsi yangu,amebadilisha mawazo yangu;halafu mawazo yangu yakawa halisi sana mpaka yakawa maneno yangu mdomoni;na yakadhihirika,na sasa ni mkristo imenifanya niwe mtu tofauti.hicho ndicho kilicho kufanya wewe.unaona?

Mungu anaponena chochote;lazima kitoke,kwa maana kwanza ni mawazoyake, halafu Neno lake lina dhihirika.halafu hakuna kitu….haijalishi kunakuja nini au kunaendelea nini,lazima

kitokee.unaweza kuona vile neno nisivyoshindwa? Oh mimi.

Kwa hiyo kama unazungumza jambo moja na kuwaza lingine,ni heri uache hilo.yaweke mawazo yako kwa Mungu,yawe safi,na ukae pamoja nalo,na uzungumze jambo lilelilewakati wote.unaona?usiseme…..vemanitasema nitaliamini hilo;ila nitaenda ili nichunguze,``liamini hilo.Amina!

Nukuu za kiingereza;
Hekima ikishindana na imani,aya157
Kristo(55-0221),phoenix),aya,E-17
Yakini uk.10-11
Neno limefanyika mwili, ripoti ya safari ya India aya172-188,213muhuri wa kwanza aya 117,uk 134.

---

*jiwe la kiroho la kujengea na 109 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe, Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*